GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam.6649 **20 Aprili, 2017** **Bei, Shs. 300,000**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya 2017 15

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya 2017

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi, katika kikao kitakachoanza tarehe 10 Mei, 2017 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
20 Aprili, 2017

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA

WA

SHERIA YA KUWEKA VIFUNGU VYA UANZISHAJI WA KODI ITAKAYOJULIKANA KAMA USHURU WA BIDHAA NA HUDUMA KWA BIDHAA NA HUDUMA ZINAZOINGIZWA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

UMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ushuru wa bidhaa na huduma Nam. … ya 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika Zanzibar kwa bidhaa na huduma zinazopaswa kutozwa ushuru kama ilivyoainishwa chini ya Sheria hii.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"ndege" inajumuisha kila aina ya ndege inayotumika kwa usafiri wa angani;

"utaratibu wa kipimo cha bei halisi" maana yake ni kipimo cha makubaliano ya kimataifa kilichokubalika katika kutambua miamala ya manunuzi na mauziano baina ya watu wanaohusiana;

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Kamishna kutekeleza majukumu yoyote chini ya Sheria hii;

"bia" inajumuisha kilevi chenye ale, pota, na kinachojumuisha bia nyengine na kilevi kinachotengenezwa na kuuzwa kama kilivyoelezwa na inayojumuisha bia kwa kiwango zaidi ya asilimia 2 za spiriti na isiyojumuisha vilevi vya kienyeji kama vilivyoainsihwa ndani ya sheria inayohusiana na pombe na vilevi;

"sigara" maana yake ni sigara, chiroti au sigarilo zilizotayarishwa kwa tumbaku;

"sigireti" maana yake ni sigara zilizotayarishwa kwa tumbaku na inajumuisha vifunganisho na karatasi za kuvutia sigara;

"Kamishna" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya 1996;

"siku" hazitajumuisha siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko;

"thamani inayotozwa ushuru" maana yake katika kuhusiana na:

(a) matumizi ya simu ya mkononi, kiwango cha malipo kinacholipwa kwa huduma ya mawasiliano ya kielektoroniki kilichochotolewa kuhusiana na matumizi ya simu ya mkononi, mezani;

(b) huduma ya mawasiliano ya kielektroniki iliyolipiwa kabla ya kutumika, thamani ya malipo inayoonekana kwenye kadi ya simu iliyouzwa;

(c) malipo ya huduma kwa ajili ya kuangalia televisheni;

(d) huduma za fedha, kiwango cha tozo na ada kinacholipwa kwa ajili ya huduma; na

(e) uingizaji wa vyombo vya ukachara utatozwa kwa kutumia kiwango cha thamani ya Forodha;

"huduma ya mawasiliano ya kielektroniki" maana yake ni aina ya huduma iliyotolewa na mtu au kampuni kwa njia ya usambazaji, kuondoa, kupokea alama au viashiria vya alama, maandishi, maumbo na sauti au taarifa za kiintelejensia ya mfumo wowote, kwa waya, muonekano au njia zozote za misuguano ambayo inajumuisha:

(a) sauti, mawasiliano ya sauti, huduma za taarifa, huduma za sauti, huduma za vidio za kuona na kusikia, miito ya redio na njia nyengine za mawasiliano ya kielektroniki zilizoibuka;

(b) huduma za simu za mezani zinazojumuisha upatikanaji wa matumizi ya mitandao ya simu iliyowashwa na isiyowashwa kwa usambazaji na uwashaji wa sauti, taarifa na huduma za kuona na kusikia, huduma za simu za kitaifa na kimataifa;

(c) huduma za simu za mkononi zinazojumuisha upatikanaji na matumizi ya mitandao inayowashwa na isiyowashwa kwa usambazaji na uwashaji wa sauti, taarifa na huduma video za kuona na kusikia na ongezeko la thamani ya kodi kwa matumizi ya miito ya mbali kwa huduma za simu za kitaifa na kimataifa;

(d) huduma za mapokezi zinajumuisha maeneo ya utoaji wa huduma ya matumizi ya nyaya, mkonga au matumizi yasiyokuwa na waya na taaluma nyengine iliyotoka au iliyokatishwa miito yenye kupita kwa muda, utozaji wa uunganishaji, upatikanaji, kusitisha simu za ndani na kimataifa kwa utozaji wa matumizi ikijumuisha nguzo, utozwaji kwa

ukodishwaji inayowaunganisha kupata huduma au njia za muunganisho wa taarifa au njia za ujumbe kwa njia ya hawala;

(e) utoaji wa huduma za usimamizi wa simu kwa ada ikijumuisha miito ya kusubiri, miito ya usoni, miito ya utambuzi, miito mingi, miito yenye kuonekanwa, mirejesho ya miito, miito ya kuonesha, miito ya kuzuiwa, mrejesho wa miito wa kujifanya wenyewe, miito ya kujibu, sauti za mawasiliano, sauti za miito tofauti na huduma za vidio kuona na kusikia kwenye mikutano;

(f) huduma ya mitandao binafsi inajumuisha utoaji wa nyaya, mkonga, zisizotumia waya au ufundi wowote wa muunganisho wa mawasiliano ya kielektroniki baina ya sehemu zilizoainishwa kwa matumizi maalum ya mteja;

(g) huduma za usambazaji wa taarifa ikijumuisha utoaji wa huduma zinazotumia nyaya au zisiotumia nyaya na huduma uliotayarishwa kwa ajili ya usambazaji maalum wa taarifa;

(h) mawasiliano kupitia nakala halisi za mawasiliano ya simu (fasimaili), sauti, hawala, simu ya maandishi na huduma nyengine za mawasiliano ya kielektroniki; na

(i) huduma nyengine ambazo zitaongezwa kila baada ya muda na taasisi za fedha au watoaji wa huduma za Mawasiliano ya simu;

“ushuru” unajumuisha uanzishaji wa tozo au kodi inayotozwa na sheria nyengine yeyote ya ushuru;

“bidhaa zinazostahili kutozwa ushuru” maana yake bidhaa zinazostahili kutozwa ushuru zinazoingizwa Zanzibar ambazo zimeainishwa katika Jadueli la kwanza la Sheria hii;

“Huduma zinazostahili kutozwa ushuru” maana yake ni huduma za ndani na zinazoingizwa zinazostahili kutozwa ushuru zilizoainshwa katika Jadueli la Pili la Sheria hii;

”Ushuru wa bidhaa na huduma” maana yake ni ushuru unaotozwa kwa bidhaa na huduma chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

“Kusafirisha nje ya nchi” maana yake katika kuhusiana na:

(a) bidhaa ni uchukuaji au kusababisha upelekaji wa bidhaa nje ya nchi Washirika;

(b) huduma ni usambazaji au kusababisha usambazaji wa huduma nje ya Zanzibar;

“huduma za kifedha” zinajumuisha mabenki, huduma za bima, uhaulishaji wa fedha na huduma nyengine za kifedha zinazotolewa na mtu yeyote kama ilivyoainishwa ndani ya Sheria hii;

“Mkuu wa Forodha” maana yake ni mtu ambae mwenye dhamana ya forodha Zanzibar;

“ungizaji” maana yake ni kuingiza au kusababisha kuingizwa kwa bidhaa au huduma ndani Zanzibar;

“muingizaji” maana yake ni mtu anaeingiza, anaesababisha kuingizwa, kupokea, kushughulikia au kutoa bidhaa au huduma ndani ya Zanzibar;

“Nahodha” anajumuishwa mtu yeyote mwenye dhamana ya usimamizi katika ndege au chombo chochote;

“Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na Fedha;

“usiku” maana yake ni muda baina ya saa sita ya mchana ya siku yeyote na saa sita ya usiku siku inayofuatia;

“vyombo kachara” maana yake ni aina zote za vyombo vilivyoainishwa chini ya Kanuni yenye kuainisha bidhaa mbalimbali na viwango vya tozo kwa bidhaa hizo zinazotumiwa na Idara ya Forodha;

“mmiliki” kwa ajili ya bidhaa zinastahili kutozwa ushuru, ndege, chombo, gari, au kitu kingine, kinachojumuisha mtu yeyote, isipokuwa afisa anaekaimu katika majukumu yake kutoka kwa mmiliki, wakala au mtu anaemiliki au mtu anaenufaika au anaesimamia au mtu mwenye uwezo wa kuuza bidhaa hiyo au nyenginezo;

“nchi washirika” maana yake ni nchi yoyote iliyopewa uanachama chini ya ibara ya 3 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

“afisa aliekasimiwa” maana yake ni afisa yoyote aliekasimiwa madaraka na Mkuu wa Forodha ambae kazi au majukumu yake anapaswa kuyatekeleza kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

“spiriti” maana yake ni spiriti ya aina yeyote na inajumuisha vinywaji vyote vilivyochanganywa na spiriti na michanganyiko yote na mjumuisho au matayarisho yaliyotayarishwa na spiriti lakini haijumuishi spiriti zisizo za asili kwa mujibu wa sheria inayohusiana na vilevi;

"tani zilizosajiliwa" maana yake ni meli zenye uwezo wa tani kama zilivyopangiwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Kanuni za Tani za Sheria za Meli za Kibiashara au ikiwa haijasajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii itakadiriwa kana kwamba imesajiliwa chini ya Sheria hiyo;

"chombo" kinajumuisha kila aina ya usafiri unaotumiwa na mtu yeyote;

"mvinyo" maana yake ni kinywaji chenye uwezo usiozidi kiwango cha nyuzi joto 50 kilichothibitishwa na kutengenezwa kutokana na matunda na sukari au matunda na sukari iliyochanganywa na vitu vyengine vinavyopelekea kufanyika kwa hali ya kubadilika na kupelekea upatikaji mvinyo;

SEHEMU YA PILI
UTOZAJI WA USHURU WA BIDHAA NA HUDUMA

Utozaji wa ushuru wa bidhaa.

4.-(1) Kwa masharti ya vifungu vya Sheria hii, uingizaji wa bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru zilizoainishwa katika Jadueli la Kwanza na huduma zinazopaswa kutozwa ushuru zilizoainishwa katika Jadueli la Pili la Sheria hii zitatozwa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa katika Jadueli la Kwanza na la Pili ya Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali, kufanya marekebisho ya Jadueli la Kwanza na la Pili ya Sheria hii endapo ataona kuna haja ya kufanya hivyo.

Uanishaji wa kiwango cha kutozea ushuru kwa bidhaa zinazo ingizwa nchini.

5.-(1) Kiwango cha kutozea ushuru kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kitakuwa ni kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia ushuru unaotakiwa kulipwa kwa uingizaji wa bidhaa hizo.

(2) Endapo Kamishna ataona, kwa sababu yoyote ile kwamba kuna udanganyifu au ukwepaji, juu ya kiwango cha kutozea ushuru kwa bidhaa yoyote iliyoingizwa ambayo haifanani na kiwango cha kutozea ushuru kwa bidhaa inayofanana na hiyo, anaweza kufanya makisio ya kiwango cha kutozea ushuru kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki.

Kiwango cha kutozea ushuru kwa huduma.

6.-(1) Kiwango cha kutozea ushuru kwa huduma kitakuwa ni:

(a) tozo, malipo au ushuru unaolipwa kwa huduma,ikiwa huduma inayotakiwa kulipwa imesambazwa na mtu aliesajiliwa kwa kipimo cha bei halisi; au

(b) bei ya soko juu ya huduma, kwa namna nyengine yoyote.

(2) Kiwango kinachotakiwa kulipwa hakitojumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani na ada zinazotozwa na taasisi za fedha na

haitojumuisha faida juu ya mkopo au marejesho ya mkopo au malipo ya bima.

(3) Endapo Kamishna ataona, kwa sababu yoyote ile kwamba kuna udanganyifu au ukwepaji, juu ya kiwango cha kutozea ushuru kwa huduma yoyote iliyoingizwa ambayo haifanani na kiwango cha kutozea ushuru kwa huduma inayofanana na hiyo, anaweza kufanya makisio ya kiwango cha kutozea ushuru kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi au kwa mujibu wa misingi ya kipimo cha bei halisi.

Ukaguzi wa kumbu-kumbu.

7.-(1) Afisa aliekasimiwa anaweza kumtaka mtu yoyote anaehusika juu ya uingizaji au utowaji wa bidhaa nje na ndani ya nchi, ubebaji, upakuaji, uingiaji wa chombo, upakiaji wa bidhaa ambazo zimeingizwa au kutolewa katika muda wowote ndani ya miaka mitatu ya tarehe iliyotolewa kutoa taarifa yoyote inayohusiana na bidhaa hizo na kumruhusu afisa aliekasimiwa kukagua na kuchukua au kutoa nakala za ankara za kodi yoyote, nyaraka za uingizaji wa bidhaa, mabuku au nyaraka nyengine zinazohusiana na uingizaji wa bidhaa hizo.

(2) Kwa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, endapo bidhaa hazijapokelewa ndani au nje ya nchi kwa tarehe ya uingizaji au utoaji wa bidhaa, afisa aliyekasimiwa atamtaka mtu huyo kutoa taarifa yoyote inayohusiana na bidhaa hizo kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi au Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Muda wa usamba-zaji na utozaji wa ushuru kwa huduma na uingizaji wa bidhaa.

8.-(1) Muda wa usambazaji wa huduma zinazotozwa ushuru utakuwa ni muda ambao:

(a) huduma imetolewa;

(b) ankara ya kodi imetolewa; au

(c) malipo yamepokelewa.

(2) Kwa uingizaji wa bidhaa, muda wa uingizaji wa bidhaa utakuwa pale ambapo bidhaa zimeingizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, ikiwa bidhaa:

(a) ipo bandarini;

(b) imetolewa ghalani;

(c) imeondolewa maeneo huru; au

(d) katika mazingira yoyote wakati bidhaa inaingizwa Zanzibar.

Udhibiti wa bidhaa zinazo tozwa ushuru.

9.-(1) Kwa masharti ya kifungu cha 11 cha Sheria hii, bidhaa zilizoingizwa nchini zitadhibitiwa na Mkuu wa Forodha wa Zanzibar mpaka ushuru wa bidhaa ulipwe au bidhaa itolewe nje ya Zanzibar, itolewe tena nje ya Zanzibar au iharibiwe.

(2) Mtu ambae atachukua au atajaribu kuchukua bidhaa zinazotozwa ushuru wakati chini ya udhibiti wa Mkuu wa Forodha wa Zanzibar atalazimika kulipa adhabu ya mara mbili ya ushuru unaopaswa kulipwa kwa bidhaa hizo.

Eneo la usambazaji wa huduma zinazo tozwa ushuru.

10. Huduma zitachukuliwa kuwa zimesambazwa ndani ya Zanzibar ikiwa:

(a) msambazaji wa huduma atakuwa na eneo la biashara hapa Zanzibar;

(b) huduma zimetolewa, zimetumika na zimefaidisha Zanzibar bila ya kuzingatia mkataba, malipo au faida iliyopatikana;

(c) usambazaji umefanyika Zanzibar, kwa muda mfupi au wakudumu, bila ya kuzingatia leseni, kibali, cheti, ruhusa makubaliano uidhinishaji au nyaraka nyengine itakayotolewa; au

(d) huduma imetolewa Zanzibar, na mtu yeyote aliye ndani au nje ya Zanzibar wakati wa utoaji wa huduma hizo.

Kukasimu kazi na majukumu.

11.(1) Kamishna anaweza kukasimu majukumu au utekelezaji wa kazi yeyote aliyopewa chini ya Sheria hii kuhusiana na usimamizi na ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa zinazoingizwa nchini zinazopaswa kutozwa ushuru kwa Mkuu wa Forodha wa Zanzibar.

(2) Kazi au mamlaka yeyote aliyopewa Kamishna chini ya sheria hii isipokuwa kazi ya usimamizi na ukusanyaji wa ushuru kwa utozaji juu ya uingizaji wa bidhaa nchini unaweza kufanywa au kutekelezwa na Kamishna au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Kamishna.

(3) Maamuzi yeyote yaliyofanywa au taarifa yeyote au mazungumzo yaliyosainiwa au yaliyotolewa na afisa yeyote aliyeidhinishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, yanaweza kufutwa au kurekebishwa na Kamishna au na afisa aliyeidhinishwa yatachukuliwa kuwa yamefanywa, yamesainiwa au yametolewa na Kamishna.

(4) Kamishna anaweza, kwa madhumuni ya usimamizi wa Sheria hii, kuagiza au kufanya matayarisho au kufunga mikataba na taasisi au mamlaka nyengine katika ukusanyaji wa ushuru chini ya Sheria hii.

(5) Mtu ambaye atakuwa ni sehemu ya mkataba au aliyepangiwa kukusanya ushuru atatekeleza kazi na majukumu yake aliyopewa chini ya Sheria hii.

(6) Kamishna anaweza kufuta ukasimishaji wa majukumu na mamlaka aliyoyatoa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki au mkataba iliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, kama ataona inafaa.

SEHEMU YA TATU
MALIPO YA USHURU

Malipo ya ushuru.

12.-(1) Malipo ya ushuru chini ya Sheria hii yatalipwa kwa Kamishna.

(2) Bila ya kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya Sheria za Forodha zinazohusiana na makadirio, malipo na ukusanyaji wa kodi za uingizaji wa bidhaa zitatumika kufanya makadirio, malipo na ukusanyaji wa kodi juu ya ushuru wa uingizaji wa bidhaa zinatozwa ushuru.

(3) Tarehe ya kufanya malipo ya ushuru yanayohusiana na:

(a) huduma zinazopaswa kutozwa ushuru za ndani zitakuwa kama zilivyoelezwa chini ya masharti yanayohusiana na malipo ya kodi chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi;

(b) uingizaji wa huduma zinazotozwa ushuru utakuwa katika muda wa uingizaji huduma;

(c) uingizaji wa bidhaa utakuwa kama ulivyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(4) Kiwango cha ukusanyaji wa ushuru kinachohusiana na uingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru kitakuwa ni kiwango kilichopo kwa bidhaa inayotakiwa kutozwa ushuru ambayo imeingizwa kwa matumizi ya ndani

(5) Endapo itatokezea ushuru unatakiwa kulipwa kuhusiana na bidhaa zozote ambazo zinazotakiwa kutozwa ushuru na ikiwa hazitambuliki katika mazingira yoyote, ushuru utakaolipwa kuhusiana na bidhaa hizo utalipwa kwa kiwango kilichokuwepo wakati wa kufanya malipo ya ushuru huo.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni chini ya Sheria hii au kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali kwa kuainisha malipo ya ushuru kwa mtu yeyote au kundi la watu wanaopaswa kulipa ushuru katika siku nyengine yoyote ukiwacha siku ambayo mtu au kundi la watu wangetakiwa kulipa ushuru.

(7) Kamishna anaweza, endapo ataridhika kwamba ni busara kufanya hivyo, ataruhusu malipo ya ushuru katika hali yoyote kulipwa muda mwengine katika kipindi kilichowekwa cha malipo chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

Mtu anayewa-jibika kulipa ushuru.

13.-(1) Ushuru unaotakiwa kulipwa chini ya Sheria hii utalipwa kwa:

(a) muingizaji aliyeingiza bidhaa mara baada ya bidhaa hizo kuondolewa chini ya dhamana ya forodha au katika muda mwengine ambao Waziri ataelekeza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

(b) bidhaa yeyote iliyoingizwa na mtu yeyote ambae amesamehewa kulipa ushuru na baadae bidhaa hiyo ikauzwa kwa mtu mwengine na muuzaji katika muda aliyouziwa bidhaa hiyo;

(c) usambazi wowote wa mawasiliano ya kielektoroniki unaotolewa na mtoa huduma za mawasiliano ya kielektroniki katika muda ambao simu ya mkononi, za mezani au kifaa chochote kinachotumika katika kuwezesha mawasiliano ya kielektoroniki kitatumika au pale ambapo malipo yamefanyika kwa huduma hiyo kwa muda wowote kitakachofanyika mwanzo;

(d) tozo au ada zilizokusanywa na taasisi za fedha au watoa wa huduma za mawasiliano ya simu juu ya uhaulishaji wa fedha na utoaji wa huduma uliofanywa na mtoa huduma;

(e) malipo yeyote yatakayofanywa kwa kuangalia televisheni za satalaiti kwa mtoa huduma muda ambao huduma imetolewa;

(f) huduma iliyoingizwa nchini na muingizaji au mpokeaji wa huduma.

(2) Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali kuhusiana na:

(a) bidhaa zozote au aina ya bidhaa au huduma zilizoainishwa katika tangazo hilo; au

(b) mtu mwengine ambae hakutajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki,

atatozwa ushuru na endapo tangazo lililofanywa kuhusiana na watu walioainishwa katika tangazo hilo watalipa ushuru unaostahili kama ilivyotakiwa kulipwa chini ya vifungu vya Sheria au Kanuni zilizofanywa chini ya Sheria hii zitatumika kwa mtu aliyetajwa kana kwamba yeye ndiye aliepswa kulipa ushuru.

Kugomboa ushuru.

1**4.-(1)** Endapo ushuru unaotakiwa kulipwa chini ya Sheria hii haukulipwa, Kamishna anaweza kugomboa ushuru huo iwapo ushuru umehusika na:

(a) uingizaji wa bidhaa nchini zinazotozwa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki; na

(b) huduma zinazotozwa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya saba ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamishna anaweza kutumia njia nyengine yeyote iliyoainishwa katika Kanuni

iliyotungwa chini ya sheria hii kwa bidhaa zinazoingizwa nchini au huduma zinazotozwa ushuru iwapo ataridhika kwamba njia hiyo itasaidia kugomboa ushuru.

Watu na Taasisi zinazosamehewa kulipa ushuru.

15. (1) Bila ya kuathiri masharti ya vifungu vya Sheria hii, watu na taasisi zilizoainishwa katika Jadueli la Tatu la Sheria hii, watasamehewa kulipa ushuru kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali na baada ya kushauriana na Kamishna, kuainisha watu na Taasisi zinazostahiki kusamehewa kulipa ushuru kama ilivyoainsihwa chini ya Jadueli la Tatu la Sheria hii.

(3) Waziri anaweza, kufanya marekebisho ya Jadueli la Tatu la Sheria hii endapo ataona inafaa.

Misamaha ya ushuru kwa bidhaa zinazo ingizwa nchini kwa ajili ya kupelekwa nje ya nchi.

16. Endapo bidhaa zinazotozwa ushuru zimeingizwa kwa njia ya hatifungani dhamana kwa:

(a) kusafirishwa nje ya nchi, kuingizwa nchini zikiwa zimeshalipiwa ushuru sehemu jirani iliyopita bidhaa au zimeshushwa kwa muda wakati zikisubiri kusafirishwa; au

(b) kuhifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya ndege au vyombo vya usafiri na itakapothibitika Kamishna ameridhia kwamba bidhaa hizo zinasafirishwa nje ya nchi au zimehifadhiwa ghalani katika hali yeyote zitasamehewa kulipiwa ushuru.

Misamaha kwa bidhaa zinazobakia kwenye chombo.

17. Bidhaa zinazotozwa kodi ambazo zimebaki kwenye chombo na zikasafirishwa nje ya nchi kwa ndege au vyombo ambavyo vimeingizia bidhaa hizo ikiwa kwa kuhifadhiwa au vyenginevyo, vimesamehewa kulipiwa ushuru.

Misamaha kwa bidhaa zilizolipiwa ushuru Tanzania Bara.

18. Endapo bidhaa zilizoingizwa nchini na kulipiwa ushuru Tanzania Bara chini ya utaratibu wa Forodha hazitatozwa ushuru iwapo zitasafiriswa kwa ajili ya matumizi ya ndani ya Zanzibar.

Marejesho ya ushuru.

19.-(1) Endapo bidhaa inayoingizwa nchini inayopaswa kutozwa ushuru imepotea au imeharibika kwa ajali ikiwa:

(a) bidhaa haijashushwa ndani ya ndege au chombo;

(b) inaondoshwa, inapakiwa, inashushwa au inapokelewa au kutolewa kutoka eneo lolote la forodha au ghalani, au

(c) sehemu yeyote ya forodha au ghalani,

kabla ya bidhaa haijatolewa katika udhibiti wa forodha na kukabidhiwa mmiliki, ikiwa Kamishna ataridhika kwamba bidhaa hizo hazitatumika Zanzibar, Kamishna anaweza kurejesha ushuru uliolipwa kuhusiana na bidhaa hizo.

(2) Marejesho ya ushuru hayatotolewa isipokuwa mtu anayelalamika awasilishe malalamiko kuhusiana na marejesho hayo katika namna iliyoelekezwa chini ya Kanuni ya Sheria hii.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali, kurejesha ushuru wote au sehemu ya ushuru uliolipwa na mtu yeyote juu ya bidhaa au huduma yeyote inayotozwa ushuru kwa kuainisha ukomo wa muda, bidhaa, huduma au masharti mengine yeyote ikiwa ataridhika kwamba kufanya hivyo ni kwa ajili ya maslahi ya umma.

Malipo ya marejesho kwa bidhaa zilizo-haribika.

20.-(1) Endapo bidhaa zilizoingizwa Zanzibar zimeharibika kabla bidhaa hizo hazijatolewa nje ya udhibiti wa Forodha, malipo ya ushuru uliolipwa unaohusiana na bidhaa hizo unaweza kulipwa kama ilivyopendekezwa na afisa aliekasimiwa baada ya kushauriana na Mkuu wa Forodha.

(2) Malipo ya ushuru yatafanywa chini ya kifungu hiki kuhusiana na bidhaa yeyote isipokuwa kama afisa aliyekasimiwa ataridhika kwamba mbebaji bidhaa au mtoa huduma ya bima amefanya malipo kwa mmliki kuhusiana na uharibifu uliotokea, malipo hayo hayatozidi, kwa namna yeyote, kiwango cha ushuru cha thamani ya bidhaa zilizoharibika.

Marejesho ya ushuru.

21.-(1) Mtu ambae anatakiwa kulipa ushuru anaweza kuomba marejesho ya ushuru wowote kwa Kamishna kwa malipo ambayo yamelipwa kimakosa au yamelipwa zaidi ya kile ambacho anatakiwa kulipa.

(2) Maombi ya marejesho ya ushuru yatafanywa kwa Kamishna katika namna inavyoelezwa na Kanuni ya Sheria hii.

(3) Endapo Kamishna ataridhika kwamba ushuru umelipwa kimakosa au umelipwa zaidi, Kamishna ataidhinisha marejesho yote au sehemu ya marejesho hayo au atatumia kulipia kodi nyengine yoyote anayodaiwa mtu huyo.

(4) Kamishna atampa taarifa ya maamuzi ya maandishi mtu aliyeomba marejesho ya ushuru ndani ya siku thelathini (30) juu ya maamuzi ya maombi ya marejesho hayo.

SEHEMU NNE
HESABU NA KUMBUKUMBU

Hesabu na kumbu-kumbu.

22.-(1) Mtu ambae anatakiwa kulipa ushuru atatakiwa kuweka kumbukumbu kama inavyotakiwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi

au Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa uingizaji wa bidhaa zinatozwa ushuru.

(2) Afisa aliyekasimiwa au afisa dhamana anaweza kwa madhumuni ya Sheria hii:

(a) bila ya taarifa ya awali ya maandishi, katika muda wowote, kuingia katika eneo lolote na kufanya ukaguzi na kuchukua maelezo kama akiona inafaa;

(b) wakati yupo katika eneo au muda wowote, atamtaka mtu yeyote kutoa buku, nyaraka au kifaa cha kielektoroniki ambacho kwa Sheria hii kinatakiwa kuhifadhiwa au kuambatanishwa au kinahusiana au anaamini kwamba kinatiliwa shaka kuhusiana uchunguzi kwa mujibu wa Sheria hii na kimo katika eneo au kinamilikiwa au kinahifadhiwa chini ya uangalizi wa mtu huyo au mfanyakazi wake;

(c) muda wowote na sehemu yeyote, atamtaka mtu yeyote ambae anaamini kwamba anamiliki au anahifadhi buku lolote, nyaraka au kifaa cha kielektroniki kinachohusiana na jambo lolote linalofanywa chini ya sheria hii; na

(d) uchunguzi na kuchukua au kutoa nakala za buku lolote, nyaraka au kifaa cha kielektroniki na atamtaka mtu yeyote kutoa maelezo ya uingizaji na anaweza kuambatanisha buku, nyaraka au kifaa cha kielektoroniki kama vitasaidia kujenga ushahidi kuhusiana na jambo lolote linalofanywa chini ya sheria hii;

(3) Mtu ambae:

(a) anahusiana na biashara;
(b) anafanya au anatumia eneo lolote; au
(c) ameajiriwa na mlipa kodi,

atamruhusu katika muda wowote afisa aliyeidhinishwa kuingia katika eneo kwa ajili kutekeleza majukumu na mamlaka yake chini ya Sheria hii.

(4) Endapo afisa aliyekasimiwa au afisa aliyeidhinishwa, na baada ya kubainisha uwezo na madhumuni yake kwamba anahitaji kuingia ndani ya eneo lolote na endapo muda ule hakuruhusiwa kuingia yeye na msaidizi wake, wanaweza muda wowote, isipokuwa wakati wa usiku awepo na afisa wa polisi:

(a) kuvunja au kufungua mlango au dirisha au kuvunja ukuta wa eneo hilo kwa madhumuni ya kuingia ndani na kufanya ukaguzi;

(b) kuvunja eneo la chini au sakafu ya eneo lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na endapo chumba, eneo, tajuri, kontena la

kuhifadhia, boksi, au kifungasho kilichofungwa kwa ufunguo na ambapo funguo hazikutolewa zilipoombwa, anaweza kufungua chumba hicho, eneo, tajuri, kontena la kuhifadhia, boksi, au kifungasho katika njia yeyote.

(5) Kamishna au Mkuu wa Forodha anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake muda wowote na katika sehemu aliyoiweka Kamishna au Mkuu wa Forodha na anaweza kumuuliza masuali mtu huyo ikiwa peke yake au mbele ya watu wengine, kama atakavyoona inafaa, kuhusiana na na jambo lolote linalofanywa chini ya sheria hii;

(6) Afisa aliyekasimiwa anaweza:

(a) kupanda meli yeyote katika eneo la bahari au la uvuvi la Zanzibar au kusimamisha na kupanda chombo chochote ndani ya Zanzibar na kufanya ukaguzi wa chombo hicho au mtu yeyote au bidhaa ambazo ushuru wake haujalipwa ikiwa kuna sababu zinazomfanya aamini kwamba kuna mambo yamefanyika ambayo yanakwenda kinyume na masharti ya Sheria na Kanuni iliyofanywa chini ya Sheria hii;

(b) ikiwa chombo chochote, chumba, sehemu ya chini ya meli, eneo, tajuri, kontena la kuhifadhia kifungasho au kontena lililofungwa ikiwa funguo zake hazikutolewa wakati zilipotakiwa, atafungua, chumba, sehemu ya chini ya meli, eneo, tajuri, kontena la kuhifadhia kifungasho au kontena katika njia yeyote;

(c) atakuwa huru kuingia na kufungua kila sehemu ya meli, ndege au chombo na kukagua bidhaa zote zilizomo ndani na maeneo ya wazi ya meli na kuweka alama au kuhifadhi bidhaa zilizomo ndani ya meli au chombo hicho ikijumuisha vifaa vilivyomo kwenye meli hiyo, na atamtaka nahodha wa meli au wa ndege au mtu yeyote mwenye dhamana na chombo hicho kutoa nyaraka yeyote inayohusiana na bidhaa hizo ambazo zinazohusiana na masharti yeyote ya Sheria hii.

(7) Afisa aliyekasimiwa na afisa dhamana anaweza kutia kufuli, lakiri, alama, kufunga au kuhifadhi ghalani, chumbani, sehemu ya chini ya meli, eneo, chombo, zana, chombo au bidhaa ikiwa kuna sababu zinazomfanya amini kwamba kuna uvunjifu wa Sheria au Kanuni umefanyika au unataka kufanyika kuhusiana na mambo hayo.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI MENGINEYO

Kuingiza bidhaa nchi kwa mara ya pili.

23.-(1) Endapo bidhaa zinazotozwa ushuru zimeingizwa nchini kwa mara pili baada ya kuzisafirishwa nje ya nchi, na ikawa hakuna marejesho ya ushuru yaliyolipwa, au ikiwa yamelipwa kwa Kamishna, bidhaa hizo

hazitotozwa ushuru, lakini ikiwa bidhaa hizo zimebadilishwa kutoka hali yake ya asili nje ya nchi na thamani yake ikawa imeengezeka, kiwango cha thamani ya bidhaa kilichoongezeka ndicho kitakachotozwa ushuru kwa mujibu wa kiwango kinachotumika.

(2) Kifungu hiki hakitotumika katika mazingira yoyote ambayo bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru zimeingizwa nchini kwa mara pili zikiwa zimechanganywa ambazo zinafanya kuwa ni sehemu moja ya bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru mpaka bidhaa zote kwa ujumla ziingizwe tena kwa mara nyengine nchini ambazo zimechanganywa kuwa ni bidhaa mbili au zaidi ambazo zimesafirishwa nje ya nchi.

(3) Kwa masharti ya Sheria hii, ushuru hautotozwa zaidi ya mara moja kuhusiana na bidhaa zozote zinazopaswa kutozwa ushuru.

Udhibiti wa Forodha kwa bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru.

24. (1) Bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru zitakuwa chini ya udhibiti wa Forodha kwa bidhaa zote zilizoingizwa ambazo:

(a) zimeingizwa nchini, kupitia Afisi ya Posta, tokea wakati wa kuingizwa mpaka kutolewa kwa matumizi ya ndani au mpaka zisafirishwe nje ya nchi;

(b) zinazohusu marejesho tokea wakati wa malalamiko ya marejesho mpaka usafirashaji wa bidhaa hizo nje ya nchi;

(c) zipo chini ya udhibiti wa afisa aliyekasimiwa zikiwa zimehifadhiwa katika eneo la Forodha zikisubiri kusafirishwa nje ya nchi;

(d) ndani ya ndege au chombo chochote wakati ikiwa zipo ndani ya eneo la bandari au sehemu yeyote ndani ya Zanzibar,

(2) Endapo bidhaa inayopaswa kutozwa ushuru ipo katika ya udhibiti wa Forodha Afisa aliyekasimiwa anaweza muda wowote kuichunguza bidhaa na mtu hatopaswa kumzuia kuchunguza bidhaa hizo wakati akitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

(3) Endapo bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru zipo chini ya udhibiti wa Forodha na zikathibitika kuwa hazifai kwa matumizi ya ndani, Kamishna, anaweza kumtaka mmiliki wa bidhaa hizo kuziharibu kwa gharama za mmiliki wa bidhaa hizo, katika namna iliyoainishwa katika Kanuni zilizofanywa chini ya Sheria hii.

(4) Kamishna anaweza kuelekeza namna ya kurejesha ushuru uliokusanywa kutokana na bidhaa hizo.

Uingizaji na uhifadhi wa bidhaa zinazotozwa ushuru.

25. Masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayohusiana na uingizaji na uhifadhi wa bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru wa Forodha zitatumika kwa uingizaji na uhifadhi wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa chini ya Sheria hii.

Bidhaa zinazochukuliwa kuwa zimeingizwa Zanzibar.

26. Kwa madhumuni ya Sheria hii bidhaa zote zinazoingizwa ndani ya Zanzibar zinachukuliwa kuwa zimeingizwa Zanzibar ikiwa:

(a) zimeingizwa ndani ya Zanzibar kwa chombo au ndege, wakati chombo au ndege hiyo ipo safari iliyokudiwa na moja kwa moja ikawasili katika eneo la udhibiti wa Forodha au wakati ikishusha bidhaa katika sehemu inayokusudiwa kushushwa Zanzibar ikiwa chombo au ndege hiyo haikufika katika safari iliyokusudiwa kushusha bidhaa au ikiwa bidhaa hizo zimezishusha kabla ya kuwasili kwa chombo au ndege katika sehemu iliyokusudiwa kushuswa bidhaa hizo;

(b) bidhaa hazijashushwa Zanzibar lakini bidhaa hizo zimeingizwa ndani ya eneo la Zanzibar kupitia chombo au ndege wakati bidhaa hizo zinatakiwa kushushwa;

(c) bidhaa zimeingizwa Zanzibar kupitia posta wakati wa uingizaji kwa mujibu wa vigezo vya aya ya (a) na (b) ya kifungu hiki kwa mujibu wa namna ya uchukuzi wa bidhaa hizo; na

(d) bidhaa zimeingizwa Zanzibar katika namna yeyote ambayo haijatajwa katika kifungu hiki katika muda ulioainishwa ndani ya Tangazo lililochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali au ikiwa muda haujaainishwa katika Tangazo hilo kuhusiana na bidhaa zenye utata muda wa uingizwaji wa bidhaa hizo utaamuliwa na Kamishna.

Wajibu wa kulipa ushuru wa bidhaa na huduma kwa mtu aliyekuwa hayupo.

27. Endapo mtu anaetakiwa kulipa ushuru wa bidhaa na huduma chini ya Sheria hii hayupo Zanzibar Kamishna anaweza, kumpa taarifa ya maandishi:

(a) wakala wa mtu huyo;
(b) mtu anaemsimamia biashara za mtu huyo ambae yupo Zanzibar na ambae anaweza kumuwakilisha mtu huyo katika jambo lolote litakalomuwajibikia kulipa ushuru;

(c) mpokeaji wa bidhaa au huduma;
(d) meneja anaehusika na biashara za mtu huyo anaehusika na ulipaji wa ushuru,

kulipa ushuru kwa niaba yake kana kwamba yeye ndie anaepaswa kulipa ushuru chini ya masharti ya Sheria hii.

Ukwepaji wa kulipa kodi.

28. Mtu aliyejiwekea utaratibu maalum kwa dhamira ya kukwepa kodi kwa lengo la kupata faida kwenye kodi na faida hiyo ikapatikana, Kamishna anaweza ndani ya kipindi cha miaka mitano tokea siku ya mwisho ya mwezi ambayo faida ya kodi aliyoipata imegundulika atamkadiria kiasi cha ushuru kinachotakiwa kulipwa kana kwamba hakuwa na dhamira ya ukwepaji wa ushuru.

Wajibu wa kulipa ushuru wa huduma na bidhaa.

29. (1) Mtu ambae anakusanya ushuru wa bidhaa na huduma unaopaswa kulipwa Zanzibar kuhusiana na miamala iliyofanyika kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii inapaswa kulipwa chini ya Sheria hii; isipokuwa ushuru uliowasilishwa kwa Kamishna au ushuru uliorejeshwa kwa mlipaji wa ushuru huo.

(2) Mtu ambae atashindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atatakiwa kulipa ushuru aliopaswa kulipa pamoja na adhabu isiyopungua shilingi Milioni Tatu na isiyozidi shilingi Milioni Kumi.

kujifanisha.

30. Mtu ambae atajifananisha na afisa aliyeidhinishwa au afisa aliyekasimiwa katika kutekeleza majukumu au mamlaka waliyopewa chini ya sheria hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua shilingi Milioni Mbili na isiyozidi shilingi Milioni Kumi au kifungo cha kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Makosa na adhabu.

31.(1) Mtu ambae:

(a) ataondoa au atajaribu kuondoa bidhaa wakati zipo chini ya dhamana ya Forodha;

(b) atashindwa kulipa ushuru wa bidhaa na huduma wakati uliopaswa kulipwa;

(c) atashindwa kuweka kumbukumbu vizuri kama inavyotakiwa chini ya Sheria hii;

(d) atamzuia au atajaribu kumzuia afisa aliyekasimiwa au afisa aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu yake;

(e) atashindwa au atakataa kutoa nyaraka au maelezo yanayotakiwa kuhusiana na bidhaa, huduma au biashara zinazopaswa kulipiwa ushuru;

(f) atashindwa kujibu masuala aliyoulizwa na afisa aliyekasimiwa au afisa aliyeidhinishwa yanayohusiana na bidhaa, huduma au biashara zinazopaswa kulipiwa ushuru;

(g) kwa makusudi anatoa maelezo au nyaraka za udanganyifu kwa afisa aliyeidhinishwa au afisa aliyekasimiwa,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya mara mbili ya ushuru unaopaswa kulipwa au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote ambae atashindwa kumjuilisha Kamishna tofauti iliyojitokeza baina ya kumbukumbu sahihi ya bidhaa zilizoingizwa chini ya udhibiti wa ushuru; au mabadiliko ya mambo ya kibiashara atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini ya Shilingi Milioni Mbili au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Makosa mengine.

32. Masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayohusiana na makosa na adhabu juu ya uingizaji wa bidhaa yatatumika kwa uingizaji wa bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru.

Adhabu ya Jumla

33. Mtu ambae atakwenda kinyume na masharti ya Sheria hii au Kanuni zake na ikiwa adhabu yake haijaainishwa, atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atatozwa faini ya shilingi Milioni Mbili au kifungo cha kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kanuni

34.-(1) Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza:

(a) kuainisha ada na tozo zinazotakiwa kutozwa kwa bidhaa zinazoingizwa na kutozwa ushuru au huduma zinazopaswa kutozwa ushuru Zanzibar;

(b) kuweka utaratibu wa kuwasilisha malipo kwa kutumia fomu maalum ambazo zitatakiwa kuainishwa chini ya Sheria hii;

(c) kuweka utaratibu wa marejesho ya malipo ya ushuru wa bidhaa na huduma;

(d) kuweka namna ya kukusanya na kuhifadhi ushuru wa bidhaa na huduma;

(e) kuainisha au kuweka utaratibu wa jambo lolote ambalo linalotakiwa kuelezwa kwa madhumuni na utekelezaji wa Sheria hii.

Kubakiza.

35. Jambo lolote lilofanywa katika kutoza ushuru wa bidhaa na huduma yeyote Zanzibar kabla ya kuanza kutumika Sheria hii litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

SEHEMU YA SITA
MAREKEBISHO YATOKANAYO

Marekebisho ya sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009.

36. Jadweli la Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009 inarekebishwa kwa kuingizwa kipengele cha 6 baada ya Kipengele cha 5 kama ifuatavyo:

"Sheria ya Ushuru wa bidhaa na huduma Nam. …..…., 2017."

Marekebishi ya Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya 1996.

37. Jadweli la Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya 1996 inarekebishwa kwa kuingizwa kipengele cha 10 baada ya Kipengele cha 9 kama ifuatavyo:

"Sheria ya Ushuru wa bidhaa na huduma Nam. ……., 2017."

JADUELI LA KWANZA

Bidhaa zinazotozwa ushuru
(Chini ya kifungu cha 4)

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
20.09		Juisi zinazoingizwa ikijumuisha juisi nzito ya zabibu na juisi za mbogamboga, zisizochanganywa na kusindikwa na spiriti, ikiwa zimechanganywa au kutochanganywa na sukari au vitu vyengine vitamu.	lita	Tsh. 210.00 kwa lita
22.02		Maji, ikijumuisha maji yenye madini na maji yenye gesi, yaliyochanganywa na sukari au vitu vyenye ladha ya utamu na vinywaji vyengine visivyo na ulevi ambavyo havijumuishi matunda au juisi za mbogamboga za kichwa cha habari Nam. 20.09	lita	Tsh. 210 kwa lita
	2202.10.00	Maji, ikijumuisha maji yenye madini na maji yenye gesi, yaliyochanganywa na sukari au vitu vitamu au vyenye ladha.	lita	Tsh. 58.00 kwa lita
	2202.90.00	---nyenginezo	lita	Tsh. 58.00 kwa lita
22.03		Bia zinazotengenezwa kwa nafaka		
	2203.00.10	---Kilevi cha stauti na pota bia zilizotengenezwa kwa mvuke zinazotokana na nafaka	lita	Tsh. 729.00 kwa lita
	2203.00.90	---nyenginezo		Tsh. 729.00 kwa lita
22.04		Mvinyo wa zabibu ikijumuishwa mvinyo unaotokana na zabibu safi inayojumuishwa na mivinyo iliyotayarishwa; juisi nzito ya zabibu isiyoainishwa katika kichwa cha habari Nam. 20.09		
		-- mvinyo mkali		
	2204.10.10	--- bia zinazotokana na zabibu zenye kiwango kinachozidi asilimia 75	lita	Tsh. 2,236 kwa lita
	2204.10.90	---nyenginezo	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita

ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
	--mvinyo mwengine; unaotokana na juisi ya nzito ya zabibu zilizosindikwa iliyozuiwa kuchanganywa na ulevi		
	--zilizohifadhiwa katika kontena zenye ujazo wa asilimia 21 au chini		
2204.21.00	---zenye kiwango cha zabibu cha zaidi ya asilimia 75	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
2204.21.00	---nyenginezo	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
2204.29.00	---nyenginezo	lita	Tsh.2,236.00 kwa lita
2204.30.00	--zenye kiwango cha zabibu kinachozidi asilimia 75	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
2204.30.00	---nyenginezo	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
	Pombe aina ya vamaus na mvinyo mwengine wa zabibu safi zenye ladha ya mti au iliyoengezwa harufu yenye ladha		
	--zilizohifadhiwa ndani ya kontena yenye zenye ujazo wa asilimia 21 au chini		
2205.10.00	--- zenye kiwango cha zabibu kinachozidi asilimia 75	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
2205.10.90	---nyenginezo	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
	--nyenginezo		
2205.90.10	--- zenye kiwango cha zabibu kinachozidi cha asilimia 75	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
2205.90.90	---nyenginezo	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
	Vinywaji vyengine zilivyosindikwa kwa mfano pombe kali, kwa mfano sida, peri, midi vilivyochanganywa na kusindikwa na mchanganyiko wa vinywaji vyengine ambavyo havikuelezwa au kujumuishwa pahala popote		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
	2206.00.10	---pombe kali aina ya sida	lita	Tsh. 2,236.00 kwa lita
	2206.00.20	Bia iliyotengenezwa kienyeji kwa kutumia nafaka kwa kiwango cha asilimia 100	lita	Tsh. 429.00 kwa lita
	2206.00.90	--nyenginezo		Tsh. 2,236.00 kwa lita
		kilevi cha ethili chenye uwezo wa ujazo usiopungua asilimia 80; spiriti, vilevi na vinywaji vyenye spiriti		
	2208.20.00	-spiriti zinazopatikana na mvinyo wa zabibu uliochujwa au juisi nzito ya zabibu zilizochujwa		Tsh. 3,315.00 kwa lita
	2208.30	- Wiski	lita	Tsh. 3,315.00 kwa lita
	2208.40.00	-pombe inayotokana na mabaki ya miwa na spiriti nyengine zinazopatikana na kwa miwa iliyosindikwa na kuchujwa	lita	Tsh. 3,315 kwa lita
22.05				
	2208.50.00	-pombe aina ya Gini na Giniva	lita	Tshs. 3,315.00 kwa lita
	2208.60.00	-pombe aina ya Vodka	lita	Tsh. 3,315.00 kwa lita
	2208.70.00	-vinywaji vikali vya Likwa na kodiali	lita	Tsh. 3,315.00 kwa lita
		-nyenginezo		
	2008.90.10	Spiriti iliyochujwa mfano wa Konyagi, Uganda waragi	lita	Tsh. 3,315.00 kwa lita
22.06	2208.90.00	--nyenginezo		Tsh. 3,315.00 kwa lita
		-siga, cheroti, sigarilo na sigireti za tumbaku au vitu vinavyojumisha tumbaku		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
		- sigireti zenye tumbaku		
	2402.20.10	---zisizokuwa na kichujio na zimejumuisha kiwango cha tumbaku kinachozidi asilimia 75	mil	Tsh. 11,854.00 kwa mil
	2402.20.90	---yenye kichujio zinazojumuisha kiwango cha tumbaku kinachozidi asilimia 75	mil	Tsh. 28,024.00 kwa mil
		---nyenginezo	mil	Tsh. 50,700.00 kwa mil
		---nyenginezo	mil	Tsh. 50,700.00 kwa
		-zinazotengenezwa kwa tumbaku na vitu vinavyojumuisha tumbaku, aina ya majani ya tumbaku ya asili yaliyosokotwa au yaliyoengezewa harufu na ladha		
		--tumbaku za kuvuta, ikiwa imejumuisha au haijajumuisha vitu vyenye asili ya tumbaku kwa kiwango chochote		
	2403.10.10	--- karatasi za kuvutia sigara / filler	kg	Ths. 25,608.00 kwa kg
	2403.11.00	--tumbaku za kuvuta ikiwa zimejumuisha au hazikujumuisha tumbaku katika utengenezaji wowote		
		--- bomba ya kuvutia tumbaku zilizoainishwa katika kichwa cha habari kidogo cha taarifa nam. 1 cha ukurasa huu	kg	30%
	2403.19.00		kg	30%
		---nyenginezo		
	2403.91.00	---nyenginezo	kg	30%
	2403.99.00	--- tumbaku ya asili iliyo hifadhiwa kwenye majani au ilizoengezewa harufu na ladha	kg	30%
		---nyenginezo		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
27.10		Mafuta aina ya petroli na mafuta yanayotokana na madini ya lami isipokuwa mafuta yaliyokuwa hayajasafishwa ambayo utayarishaji wake haujaelezewa au kujumuishwa popote, wenye uzito wa asilimia 70 au zaidi kwa mafuta ya petroli au mafuta yanayotokana na madini ya lami, mafuta kimsingi yanajumuisha utayarishwaji wake wa mafuta machafu		
		-mafuta mepesi na utayarishaji wake		
	2710.11.10	---mafuta ya spiriti ya kawaida	lita	Tsh.135.00 kwa lita
	2710.11.20	---mafuta ya spiriti mazito	lita	Tsh.146.00 kwa lita
		mengineyo		
		-mafuta ya kati na utayarishaji wake		
		-utayarishaji		
	2700.19.21	----aina ya mafuta ya kuendeshea ndege	lita	hakuna
	2700.19.22	----mafuta ya kuwashia taa	lita	Tsh.122.00 kwa lita
	2700.19.29	----mafuta ya kati na utayarishaji	lita	Tsh.8.7145 kwa lita
		--mafuta ya gesi na dizeli		
	2710.19.31	-mafuta ya gesi yanayotumika kwa kuendeshea vyombo, taa na injini zenye mwendo wa kasi	lita	Tshs.127.00 kwa lita
	2710.19.32	----mafuta ya dizeli yanayotumika viwandani, ingini za baharini na zinazofanya kazi bila ya kuondoshwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine	lita	Tsh.201.00 kwa lita
		-mabaki ya mafuta		
	2710.19.41	---- mabaki ya mafuta kwa vyombo vya baharini, vya kuleta joto na mafuta yanayofanana nayo yenye kipimo cha sentistoki 180	lita	Tsh. 97.00 kwa lita

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
	2710.19.42	----mabaki ya mafuta kwa vyombo vya baharini, vya kuleta joto na mafuta yanayofana nayo yenye kipimo cha sentistoki 180	lita	Tsh. 97.00 kwa lita
	2710.19.43	----mabaki ya mafuta kwa vyombo vya baharini, vya kuleta joto na mafuta yanayofanana nayo yenye kipimo cha sentistoki 280	lita	Tsh. 97.00 kwa lita
	2710.19.49	----mabaki ya mengine ya mafuta	lita	Tsh. 97.00 kwa lita
	2710.19.51	-mengineyo	lita	Tsh. 500 kwa m3
	2710.19.52	----mafuta ya kulainishia mashine	lita	Tsh. 0.75 kwa kg
27.11		----girisi ya kulainishia mashine		
	2711.11.00	-gesi ya petroli na gesi nyengine za haidrokabon	kg	Tsh.114.00 kwa kg
		--gesi asili		
	2711.12.00		kg	Tsh.114.00 kwa kg
		--Propeni		
	2711.13.00		kg	Tsh.114.00 kwa kg
		--Buteni		
	2711.14.00		kg	Tsh.114.00 kwa kg
		--Ethilini, propilini, butilini na butadieni		
	2711.19.00		kg	Tshs.114.00 kwa kg
39.23		--mengineyo		
		Vitu vinavyotumika kusafirishia au kuhifadhia bidhaa za plastiki, vifungio, mifuniko ya plastiki		
	3923.21.00	-mifuko na mabegi ikijumuisha vitu vya kuhifadhia mikoba na mifuko	kg	120%
	3923.21.10	-yenye polimasi ya ethilini	kg	120%
		---mikoba ya kwendea dukani		
	3923.29.10	--Mengine ya plastiki	kg	120%
		---mikoba ya kwendea dukani		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
85.23				
		Diski na kanda, na vifaa vya kuhifadhia, kadi za miamala na zana nyengine za kurikodia sauti au matukio ikiwa yamehifadhiwa au hayajahifadhiwa ikijumuisha habari vifaa vya kutengenezea diski		
		- Vifaa vya Sumaku vya kunasia habari		
	8523.29.90	- Zisizorikodiwa	u	Tsh. 50.00 kwa uniti
		--kanda za kuona na kusikia zilizorikodiwa		
	8523.40.90	Vifaa vya kuonea habari	u	Tsh. 50.00 kwa uniti
		DVD, VCD, CD zilizorikodiwa		
87.02				
		Vyombo vya moto vya kusafirishia watu kumi au zaidi ikijumisha dereva		10%
	8702.10.20	- Chenye nguvu za muwako kwenye injini inayotumia dizeli au sehemu ya dizeli		
		--chenye uwezo wa ujazo wa kiwango cha 2000 cc au chenye uwezo wa kubeba watu wasiozidi kumi		
		-vyenginevyo		
87.03				
		Gari na vyombo vyengine vya moto mahsusi vilivyoundwa kwa kwa ajili ya usafirishaji wa watu isipokuwa zile zilizoainishwa katika kichwa cha habari Nam. 87.02 ikijumuisha gari aina ya stesheni wagoni na gari zinazotumika katika mashindano ya mbio za gari		
	8703.22.90	--vyombo vyengine vya moto vyenye kutoa miwako na miripuko ya moto kutoka kwenye injini	u	5%
		---vyenginevyo		
	8703.23.01	-- zenye uwezo wa kupitisha na kuhifadhi unaozidi cc 1,500 na usiozidi cc 3,000	u	5%
		--zenye uwezo wa kupitisha na kuhifadhi unaozidi cc 1,500 na usiozidi cc 2,000		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
	8703.23.99		u	10%
		-----vyenginevyo		
	8703.24.90	--- zenye uwezo wa kupitisha na kuhifadhi unaozidi cc 3,000	u	10%
		-----vyenginevyo		
		- Vyombo vyengine vya moto vyenye nguvu za muwako kwenye injini inayotumia dizeli au sehemu ya dizeli		
	8703.31.91	- zenye kupitisha na kuhifadhi uwezo usiozidi cc 1,500	u	Hakuna
	8703.31.99	--- zenye kupitisha na kuhifadhi uwezo usiozidi cc 1,000	u	5%
		--- -vyenginevyo		
	8703.32.91	-- zenye kupitisha na kuhifadhi uwezo unaozidi cc 1,500 na usiozidi cc 2,500	u	5%
	8703.32.99	---- zenye kupitisha na kuhifadhi uwezo unaozidi cc 1,500 na usiozidi cc 2000	u	10%
		-----vyenginevyo	u	5%
	8703.33.90	-- zenye kupitisha na kuhifadhi uwezo unaozidi cc 2,500	u	10%
		----vyenginevyo		
88.02		Ndege nyengine kwa mfano helikopta, ndege za abiria, ndege zinazotumika kwa ajili ya uchunguzi wa mambo ya anga zikiwemo satalaiti na sabobitali na ufunguzi wa ndege zinazotumika kwa ajili ya uchunguzi mambo ya anga kwa matumizi binafsi ispokuwa kwa ndege za kibiashara		
	8802.11.00	-helikopta	u	20%
	8802.12.00	----zisizokuwa na ujazo wa uzito usiozidi kg 2,000	u	20%
	8802.20.00	--zisizokuwa na ujazo wa uzito unaozidi kg 2,000	u	20%
		--ndege za abiria na ndege nyengine		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
		zisizokuwa na ujazo wa uzito usiozidi kg 2,000		
	8802.30.00		u	20%
	8804.40.00	-- ndege za abiria na ndege nyengine zisizokuwa na ujazo wa uzito unaozidi kg 15,000	u	20%
		-- ndege za abiria na ndege nyengine zisizokuwa na ujazo wa uzito unaozidi kg 2,000 na usiozidi kg 15,000		
	9401.30.00	Viti vilivyoingizwa ndani ikiwa vinabadilishika kuwa kitanda au havibadilishiki na vifaa vyake	u	20%
	9401.40.00	--viti vya kuzunguka pamoja vyenye kuweza kushuswa na kupandishwa	u	20%
		--viti vyengine isipokuwa vya bustanini au vifaa vya kuweka kambi vinavyoweza kubadilika kuwa kitanda		
	9401.51.00	---viti vilivyotengenezwa kwa mianzi au vifaa vinavyofanana na mianzi	u	20%
	9401.59.00	---vya mianzi	u	20%
		---vyenginevyo		
	9401.61.00	--- viti vyengine vilivyotengenezwa kwa fremu za mbao	u	20%
	9401.69.00	---virefu	u	20%
		---vyenginevyo		
	9401.71.00	---viti vyengine vilivyotengenezwa kwa fremu za chuma	u	20%
	9401.79.00	------virefu	u	20%
	9401.80.00	---vyengine	u	20%
	9401.90.00	---viti vyengine	kg	20%
		vifaa		
	9403.10.00	Samani nyengine zinazoingizwa na vifaa vyake	kg	20%
		-samani za aina ya chuma zinazotumika ofisini		

MADA	ALAMA ZA HS	MAELEZO	KIPIMO	KIWANGO
	9403.20.00		u	20%
	9403.30.00	-samani nyengine za chuma		20%
	9403.40.00	-samani za aina ya mbao zinazotumika ofisini	u	20%
	9403.50.00	- samani za aina ya mbao zinazotumika jikoni	u	20%
	9403.60.00	- samani za aina ya mbao zinazotumika chumbani	u	20%
	9403.70.00	- samani nyengine za mbao	kg	20%
		-samani za plastiki		
	9403.81.00			
	9403.89.00	----samani za vifaa vyengine vikijumuisha mianzi au vifaa vinavyofanana na mianzi	kg	20%
	9403.90.00	---zilizotengenezwa kwa mianzi	kg	20%
		--nyenginezo	kg	20.kg
		-vifaa	u	25%
		--uingizaji wa vyombo kachara kuanzia miaka kumi au zaidi tokea mwaka vilivyotengenezwa vifaa hivyo	u	25%
		---uingizaji wa zana za matengenezo zilizotumika, vyombo vya moto, baiskeli, vyombo vya maringi mawili au matatu na vifaa vya majumbani vilivyotumika zikiwemo jokofu, mashine za kufulia, majiko ya kupikia, maikrowevu, mashine za kusafishia, uzio wa umeme, kipoza hewa, vipoza moto vya umeme na vifaa vyengine vinavyofanana na hivyo, vifaa vya umeme zikijumuisha televisheni, vifaa makusudi vya wino kwa mashine za uchapaji, mashine za kuchapa nakala, simu za mkononi na vyengine vinavyofanana na hivyo,		

JADUELI LA PILI

HUDUMA ZINAZOTOZWA USHURU
[Chini ya kifungu cha 4]

Nam.	MAELEZO YA HUDUMA	KIWANGO CHA USHURU
1.	Huduma za mawasiliano ya kielektroniki	Asilimia 17 ya thamani inayotozwa
2.	Huduma inayolipwa kwa kuangalia televisheni inayotolewa na watoa huduma za televisheni waliosajiliwa au watoa huduma za televisheni zinazosambazwa kwa waya zisizokuwa za Serikali Kuu au Mamlaka ya Serikali za Mitaa.	Asilimia 5 ya thamani inayotozwa
3.	Huduma zinazotolewa na Taasisi za Fedha.	Asilimia 10 ya tozo au ada iliyolipwa na mtu aliyepokea huduma
4.	Huduma za uhaulishaji wa fedha na malipo ya huduma yaliyotolewa na mtoa huduma wa mawasiliano ya simu.	Asilimia 10 ya tozo au ada iliyolipwa na mtu aliyepokea huduma
5.	Huduma nyengine zinazoingizwa nchini.	Asilimia 12 ya thamani inayotozwa

JADUELI LA TATU

WATU NA TAASISI ZINAZOSAMEHEWA KULIPA USHURU
[Chini ya kifungu cha 15]

Nam.	WATU NA TAASISI ZINAZOSAMEHEWA KULIPA USHURU
1.	Bidhaa au huduma zilizoingizwa au kununuliwa nchini na Ubalozi au Taasisi za Kibalozi.
2.	Bidhaa au huduma zinazoingizwa au kunuliwa nchini na Serikali za Nchi za Kigeni, Taasisi za Kimataifa au Mashirika yanayotoa Misaada.
3.	Bidhaa zinazotozwa ushuru ikijumuisha magari yanayoingizwa nchini na raia wanaorejea nchini.